MWONGOZO WA MATUMIZI YA MFUMO WA VIDEO CONFERENCE KATIKA TAASISI ZA SERIKALI

Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Utangulizi

- Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamebadilisha namna ya uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hivyo Serikali inachukua hatua madhubuti ikiwamo kutunga sera, miongozo, nyaraka mbalimbali ili kuendana na mabadiliko hayo.
- Moja ya hatua hizo ni Waraka wa Utumishi Na. 5 wa Matumizi Bora na Salama ya Vifaa na Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini wa Mwaka 2009.

Utangulizi ….

- Waraka Na. 5 pamoja na mwongozo wa matumizi bora, sahihi na salama ya vifaa na mifumo ya TEHAMA haukuainisha matumizi ya “Video Conference”
- Serikali imeona ni vyema kutoa Mwongozo mahsusi wa matumizi ya mfumo wa “Video Conference” katika taasisi za Serikali.

Maana ya ‘Video Conference’

- Mawasiliano kwa njia ya video (Video Conferencing) ni teknolojia inayowawezesha wahusika kutoka sehemu mbalimbali kuwasiliana kwa njia ya sauti na video hivyo kuwezesha wahusika kuonana na kusikilizana pasipo kukutana sehemu moja.
- Baadhi ya shughuli zinazoweza fanyika kwa kwa njia ya video ni mikutano ya kawaida, vikao, makongamano, midahalo, mafunzo, usaili na majadiliano ya aina mbalimbali.

Lengo la Mwongozo

- Mwongozo huu unatoa utaratibu wa kuzingatiwa katika matumizi ya mawasiliano kwa njia ya video na viwango vya vifaa vinavyohusiana na teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya video.

Faida kwa Serikali

- Kuongeza tija na ufanisi katika utekelaziji wa majukumu ya siku hadi siku.
- Kupunguza gharama za kuendesha mikutano, mafunzo na makongamano kwani haitamlazimu mjumbe wa mkutano kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine

Walengwa wa Mwongozo

- Walengwa wa mwongozo huu ni Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za mikoa, Taasisi za Umma, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Watumishi wa Umma.

Mwongozo

- Mwongozo huu una sura nne (4),
  I. Vifaa na mazingira wezeshi ya kuendesha mikutano, semina au warsha kwa njia ya video;
  II. Maandalizi ya mikutano, semina au warsha kwa njia ya video;
  III. Uratibu na ushauri wa matumizi ya mfumo wa video katika taasisi za umma.
  IV. Utaratibu unaopaswa kufuatwa wakati wa kuendesha mikutano, semina au warsha kwa njia ya video;

Sura ya Kwanza

- Aina a vifaa na miundombinu inavyohitajika kwa ajili ya mfumo wa video conference

- ✓ **Video Conferencing Codec”**
- ✓ **Kamera, Vinasa Sauti na Vipaza Sauti (camera, microphone and speaker**
- ✓ **Vifaa vya kuonesha picha (runinga, “projector” n.k)**
- ✓ **Mtandao wa mawasiliano ya Intaneti**

Sura ya Kwanza …

- Mazingira ya ukumbi au sehemu ya kuendesha mikutano kwa mfumo wa video conference
- Ukumbi au sehemu inayotumika kufanya mawasiliano kwa njia ya video inapaswa kuwa na sifa zifuatazo:
  - Hali ya joto kati ya nyuzi joto 21 mpaka 23 sentigredi;
  - Kusiwe na mwanga wa jua kutoka nje unaoingiliana na kamera;
  - Mwanga wa taa uwe ni wa kutosha na usimulike moja kwa moja upande kamera ilipo;
  - Kuta za chumba cha mkutano ziwe na rangi ya bluu mpauko (light sky blue - #82CAFA) au rangi ya samawi (Brown-#C77818); na
  - Viti vya ukumbi au sehemu inayotumika kufanya mawsiliano kwa njia ya video vipangwe katika mpangilio unaowawezesha washiriki wote kufikiwa na kamera.

Sura ya Pili

- Muandaaji wa mkutano awasiliane na Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) siku 2 kabla ya Mkutano.
- Kushirikiana na TaGLA kufanya majaribio ya awali
- Muandaaji atawajibika kutoa taarifa TaGLA pindi panapotokea mabadiliko yoyote kuhusu mkutano uliopangwa.
- Vituo vinavyohusika viunganishwe saa moja kabla ya mkutano kuanza ili kuhakiki mifum`o ya sauti, mwanga na intaneti kama inafanya kazi vizuri kabla ya mkutano kuanza

Sura ya Tatu

- Taasisi zinatakiwa kuwasiliana na TaGLA kwa msaada wa kiufundi na ushauri wa kiutaalam kwa masuala ya mikutano kwa njia video
- Wataalam wa TEHAMA wa taasisi husika watakua wasimamizi na waendeshaji wa vifaa vya video conference.
- Utunzaji na matumizi ya vifaa vya video conference uzingatie muongozo wa mtumizi bora, sahihi, na salama ya vifaa na mifumo ya TEHEMA Serikalini wa Julai 2012
- Wataalam wa TEHEMA watoe mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mfumo wa video conference ili mfumo huu uweze kuleta tija na ufanisi Serikalini.

Sura ya Nne

- Wataalam wa TAHEMA watoe maelekezo kwa washiriki jinsi ya kuendesha na kushiriki mikutano kwa njia ya video kabla ya mkutano
- Mikutano kupitia mfumo wa video conference ifuate sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji wa mikutano katika Utumishi wa Umma.
- Endapo itatokea muda uliopangwa kufanya mkutano umemalizika kabla ya mkutano husika kukamiliaka, muandaaji awasiliane na TaGLA uwezekano wa kuongeza muda

Hitimisho

- Kuwa na mfumo wa video conference bila mtandao ni sawa na kuwa na simu bila namba za kupiga.
- TaGLA itakua kama kiunganishi muhimu kwa taasisi za serekali kila zinapotaka kufanya mikutano kwa njia ya video. Hii itasaidia kuokoa pesa kwa kila taasisi kununua kifaa chake na mwisho kushindwa kukitumia ipasavyo, pia itasaidia kufanya vifaa hivi vitumike kwa ufasaha na kuleta tija